# HABARI na MATUKIO

Toleo Na. 9 | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority | tfra_official | tfra_official | Novemba 2022

JARIDA LA KILA MWEZI LA MAMLAKA YA UDHIBITI WA MBOLEA TANZANIA

# Songwe yabeba maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani kitaifa, tuzo zatolewa

**Wananchi wajengewa uwezo wa matumizi sahihi ya mbolea na kulima kwa kufuata kanuni bora za kilimo**



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stepan Ngailo akizungumza na wananchi waliohudhuria hafla ya maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Kimondo- Vywawa Mkoani Songwe tarehe 13 Oktoba, 2022.

NDANI>>

MBOLEA YA RUZUKU KUFIKISHWA WALIPO WAKULIMA 7

ONGEZENI KASI KUSAMBAZA MBOLEA - MASSAWE 9

Mkuu wa Mkoa Kigoma aipongeza TFRA kutatua changamoto uchache wa mawakala mbolea za ruzuku 11

# Songwe yabeba maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani kitaifa, tuzo zatolewa

Wananchi wa Mkoa wa Songwe na Tanzania kwa ujumla wametakiwa kutumia vema fursa inayotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Samia Suluhu Hassan ya mbolea za ruzuku katika kuzalisha mazao kwa tija na kuleta mapinduzi ya kilimo huku wakulima wakitakiwa kuhakikisha wanajisajili ili kuweza kunufaika na mpango wa mbolea hizo za ruzuku zinazotolewa msimu wa kilimo wa 2022/2023.



Mkuu wa Mkoa wa Rukwa Queen Sendiga akizungumza na hadhira iliohudhuria hafla ya maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Kimondo- Vywawa Mkoani Songwe tarehe 13 Oktoba, 2022.

Wito huo unatolewa na Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Queen Sendiga kwa Niaba ya Waziri wa Kilimo Hussein Bashe aliyekuwa mgeni rasmi wakati wa kufunga maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyobebwa na kauli mbiu "Ajenda 10/30; Matumizi sahihi ya mbolea ya RUZUKU kwa Kilimo chenye tija".

Akizungumza wakati wa hafla hiyo iliyofanyika katika viwanja vya Kimondo mkoani Songwe Mkuu wa Mkoa Sendiga anasema, lengo la Serikali la kutoa ruzuku za mbolea ni kupunguza makali ya bei ya mbolea kwa wakulima ili waweze kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo, kuimarisha usalama wa chakula nchini na kuongeza mchango wa sekta ya kilimo katika pato la taifa.

Anasema, katika kuhakikisha utekelezaji wa mpango wa ruzuku unapunguza mianya ya udanganyifu na kuweka mchakato mzima wa utoaji ruzuku kwa wakulima, Serikali imeweka mfumo wa kielektroniki ambao unaratibu utambuzi wa washiriki, usambazaji wa mbolea, mauzo ya mbolea na malipo ya fedha za ruzuku kwa kampuni zinazoingiza mbolea nchini na hivyo kuweza kufuatilia hatua moja baada ya nyingine ya usambazaji wa mbolea za ruzuku nchini lengo ikiwa kumnufaisha mkulima halisi.

Akitoa historia ya namna serikali inavyojikita katika kuongeza jitihada za kuhakikisha Tanzania inakuwa miongoni mwa nchi zinazojitosheleza kwa chakula duniani Sendiga anasema juhudi hizo zilianza tangu nchi ilipopata uhuru wake mwaka 1961 ambapo muasisi wa Taifa, Hayati Mwl. Julius Kambarage Nyerere alikuwa akisisitiza watanzania kujikita katika kilimo bora kwa ajili ya maendeleo yao binafsi na Taifa hasa katika Azimio la Iringa katika sera yake ya

# Songwe yabeba maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani kitaifa, tuzo zatolewa

Siasa ni kilimo.

Sendiga anasema, miongoni mwa changamoto kubwa katika kilimo cha nchi yetu ni tija ndogo katika uzalishaji inayosababishwa matumizi madogo na yasiyo sahihi ya mbolea, matumizi ya mbegu na zana duni za kilimo na mabadiliko ya tabia nchi.

"Utoaji wa mbolea ya ruzuku iliyotolewa na Serikali pamoja na upatikanaji wa mbegu bora na kuimarishwa huduma za ugani kutaongeza uwezo wa mkulima kuzalisha kwa tija" Sendiga anaongeza.

Kufuatia kuwa, serikali inatambua umuhimu wa Mkulima kupata mbolea kwa wakati na kwa bei anayoweza kuimudu, inasimamia kwa karibu na kufanya mazungumzo na wafanyabiashara wa mbolea ili waagize mbolea ya kutosha na kuisambaza kwa wakulima pande zote za nchi kwa msimu wote wa kilimo.

Akielezea chimbuko la Maadhimisho ya Siku ya Mbolea Mkuu wa Mkoa Sendiga anasema ni kumbukizi ya uvumbuzi wa mbolea aina ya Amonia uliofanywa na Bw. Fritz Haber mwaka 1908 ambao ulichochea mapinduzi ya kijani katika karne ya 20 na kusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza janga la njaa katika nchi nyingi duniani. Pia siku hii ya mbolea duniani inafanyika katika juma moja na siku ya chakula duniani ambayo pia inasisitiza uwepo wa chakula bora na cha kutosha kwa kila mtu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stepan Ngailo akizungumza na wananchi waliohudhuria hafla ya maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Kimondo-Vywawa Mkoani Songwe tarehe 13 Oktoba, 2022.

Akizungumza wakati akifungua maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika tarehe 11 Oktoba, 2022, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Waziri Waziri Kindamba anasema usalama wa chakula ndio usalama mkuu kuliko usalama mwingine wowote kwani bila chakula hakuna chochote kinachoweza kufanyika.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stepan Ngailo anasema lengo la kuadhimisha Siku ya Mbolea Duniani kwa mwaka 2022 ni kuwaleta pamoja wadau wa mbolea wapatao 31 ambao wameweza kuonesha bidhaa zao za mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo.

Anawataja wadau hao kuwa ni pamoja na wakulima, kampuni za mbolea, wazalishaji wa mbolea nchini,

# Songwe yabeba maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani kitaifa, tuzo zatolewa

wasindikaji wa mazao, taasisi za Utafiti wa kilimo, vyuo vya elimu ya juu, taasisi za serikali na za kiraia na anawashukuru kwa ushiriki ulioleta ufanisi katika kuadhimisha siku hiyo muhimu kwa tasnia ya mbolea nchini.

Anaendelea kusema kauli mbiu ya Siku ya Mbolea kwa Mwaka 2022 inaendana na jukumu kubwa la TFRA ambalo ni kusimamia ubora wa mbolea na kuwezesha upatikanaji wa mbolea bora kwa wakulima na kisha kuongeza tija ya uzalishaji kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya chakula na malighafi za viwanda nchini na hata nje ya Tanzania.



Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Waziri Waziri Kindamba akipokea tuzo ya Mkoa mwenyeji yalikofanyika maadhimisho ya Siku ya Mbolea Kitaifa akiwa ni mwenyeji wa maadhimisho hayo

Aidha, Dkt. Ngailo anaeleza majukumu ya Mamlaka kwa mujibu wa kifungu cha 4(1) cha Sheria ya Mbolea ya Mwaka 2009, kuwa ni kusimamia na kudhibiti ubora wa mbolea nchini,kudhibiti uzalishaji, uingizaji na biashara ya mbolea nchini, kutoa ushauri wa kitaalam kwa Serikali na taasisi nyingine juu ya masuala yanayohusu sera za usimamizi na udhibiti wa ubora na biashara ya mbolea na mwisho kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kuelimisha umma juu ya matumizi sahihi ya mbolea.

Mwisho maonesho hayo yaliambatana na utoaji wa tuzo mbalimbali kwa washiriki kwa makundi sita ikiwa ni kundi la wazaishaji wa mbolea ngumu ambapo kampuni la YARA Tanzania Limited ilichaguliwa kuwa mshindi wa tuzo hiyo, Kundi la Wazalishaji wa mbolea za maji ambapo Isacha Feeder's International Co.Ltd ilichaguliwa kuwa mshindi wa tuzo hiyo, aidha Tuzo ilitolewa kwa msambazai mkubwa wa mboea kitaifa na ETG Inputs (T) LTD kuchukua tuzo hiyo.

Tuzo nyingine zilizoshindaniwa ni mshiriki bora katika mpango wa ruzuku kwa mwaka 2022/2023 ambapo kampuni la OCP Tanzania Limited ilichaguliwa kuwa mshindi wa tuzo hiyo na mwisho ni tuzo kwa mwoneshaji bora wa maadhimisho iliyogawanywa katika makundi matatu ya uande wa vyama vya ushirika, kampuni na mabenki ambapo Guavay Company Limited ilichaguliwa kuwa mshindi, kundi la pili ni la Halmashauri za Wilaya zilizoshiriki ambapo Halmashauri ya Mji Tunduma ilipata tuzo hiyo na mwisho ni kundi la Taasisi za Serikali na Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania (TOSCI) ilishinda tuzo hiyo.












Matukio mbalimbali katika picha yakiwemo ya kutolewa kwa tuzo na huduma ya ununuzi wa mbolea iliyotolewa kwa wakulima










Matukio mbalimbali katika picha yakiwemo ya kutolewa kwa tuzo na huduma ya ununuzi wa mbolea iliyotolewa kwa wakulima

# Mbolea ya ruzuku kufikishwa walipo wakulima

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa Majaliwa amewataka wakulima nchini kujipanga kulima kwa tija na kubainisha serikali imeweka mipango mahususi kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo ya mbolea kwa wakati na kwa bei himilivu.

Amewahakikishia wakulima wanaofanya shughuli zao za kilimo mbali na maeneo ya mijini kuwa, makampuni ya mbolea yameelekezwa kuhakikisha wanakuwa na mawakala wenye uwezo wa kusambaza mbolea katika maeneo waliyopo wakulima ili kuwapunguzia mzigo wa kwenda mwendo mrefu kufuata bidhaa hiyo.



Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa Majaliwa akijibu hoja za wabunge akiwemo Mbunge wa Songea Vijijini Jenista Mhagama na Mbunge wa Madaba Josephy Mhagama juu ya utekelezaji wa mpango wa ruzuku na kueleza juhudi zinazofanywa na Serikali za kuhakikisha mbolea inafikishwa alipo mkulima. Ametoa kauli yake akizungumza na hadhira iliyoshiriki uzinduzi wa hospitali ya Wilaya ya Madaba uliofanyika tarehe 19 Oktoba, 2022 Mkoani Ruvuma.




Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (mwenye kofia nyeupe) akifuatilia tukio la uzinduzi wa hospitali ya Wilaya ya Madaba uliofanywa na Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania leo tarehe 19 Oktoba, 2022

Waziri Mkuu Majaliwa ametoa kauli hiyo leo, tarehe 19 Oktoba, 2022 alipokuwa akiihutubia hadhira iliyoshiriki hafla ya uzinduzi wa Hospitali ya Wilaya ya Madaba kwa lengo la kuwapunguzia wananchi kadhia ya kwenda mwendo mrefu ili kupata huduma za afya.

Amesema, mahitaji ya mbolea kwa mkoa wa Ruvuma ni tani elfu sitini na saba (67000) na kubainisha kuwa mpaka sasa tani 2467 zimesambazwa kwa wakulima na kwenye maghala kuna kiasi cha tani elfu moja na laki tano kwa ajili ya matumizi ya wakulima wa mkoa huo

# Mbolea ya ruzuku kufikishwa walipo wakulima

Aidha, Waziri Mkuu Majaliwa amesema zaidi ya tani elfu hamsini zinashushwa bandarini huku tani elfu ishirini na tatu zikitarajiwa kushushwa ifikapo Novemba tarehe 22, 2023 na baadaye kusambazwa katika maeneo mbalimbali nchini Ruvuma ikiwemo.

Majaliwa ameendelea kusema mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa inayotegemewa kwa uzalishaji wa chakula na kueleza mbolea kutofika Ruvuma ni kukaribisha njaa nchini jambo ambalo halikubaliki.

“Niwahakikishie wananchi wa Madaba na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla kuwa mbolea zitaletwa jipangeni tunawategemea sana kwa ajili ya kupata chakula” Majaliwa amesisitiza.

Aidha, Majaliwa ametaja kampuni za uingizaji wa mbolea nchini zinazosambaza pembejeo ya mbolea katika mkoa wa Ruvuma kuwa ni pamoja na Mohamed interprises LTD, YARA Tanzania LTD, OCP, na Premier na kubainisha kuwa mazungumzo yamefanyika kuhakikisha wanakuwa na mawakala wa kutosha watakaofikisha mbolea karibu na wakulima.

Kwa upande wao Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama na Mbunge wa Madaba Josephy Mhagama walieleza changamoto ya mawakala kupatikana mbali na maeneo yenye wakulima jambo lililotolewa ufafanuzi na Waziri Mkuu Majaliwa.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mbunge wa Songea Vijijini Jenista Mhagama akizungumza jambo wakati wa hafla ya uzinduzi wa hospitali ya wilaya ya madaba uliofanywa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa Majaliwa (hayupo pichani) tarehe 19 Novemba 2022.

# Ongezeni kasi kusambaza mbolea - Massawe

Katibu Mkuu wizara ya Kilimo Bw. Andrew Massawe amewataka wafanya biashara wote wa mbolea nchini kuongeza kasi ya kusambaza pembejeo hiyo muhimu ili iwafikie wakulima kwa wakati.

Bwana Massawe amesema hayo jana tarehe 19.10.2022 jijini Dar es Salaam alipokutana na waagizaji wa mbolea kwa lengo la kutathmini kwa pamoja utekelezaji wa mpango wa utoaji wa mbolea za ruzuku kwa msimu wa Kilimo wa 2022/2023.

Katibu Mkuu huyo amesema hali ya usambazaji wa mbolea katika maeneo mengi ya pembezoni mwa nchi hairidhishi ambapo tayari msimu wa kilimo umeshaanza.

“Suala la kufikisha mbolea kwa wakulima kwa wakati linaendana na msimu, hivyo ni muhimu kwa makampuni na mawakala wa mbolea kufanya kila linalowezekana kuwafikia wakulima kwa wakati”, Alisema Bw. Massawe.

Massawe aliyataja maeneo ambayo yana mawakala wachache wa mbolea kuwa ni Mara, Kagera, Geita , Nkasi, Kalambo, Meatu, Itilima, Busega, Maswa, Momba, Kiteto na Babati.

Aliongeza kuwa maeneo mengine yenye mawakala wachache ni Nyasa, Tunduru, Lindi, Pwani, Siha, Hai, Mwanga, Same Moshi, Longido, Monduli, Simanjiro Arumeru , Makete,



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo Gerad Mweli akifafanua jambo wakati wa kikao cha wafanyabiashara wa mbolea kilichofanyika jijini Dar es Salaam.

# Ongezeni kasi kusambaza mbolea - Massawe



Wafanyabiashara wa mbolea wakiwa katika kikao cha pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Andrew Massawe kilichofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Wizara ya kilimo, Jijini Dar es Salaam.

Ludewa, Mbarali, Chunya na Shinyanga.

Kufuatia uhaba wa wasamvazaji wa mbolea katika maeneo hayo Massawe ameyataka makampuni ya mbolea kuhakikisha wanafikisha huduma katika maeneo hayo ndani ya wiki moja ili kuwawezesha wakulima waweze kupanda mazao yao kwa wakati.

Akizungumza kwa niaba ya makampuni ya mbolea, mwakilishi wa Kampuni ya Yara, Januari Fabian aliiomba serikali kuwawezesha kupata usafiri wa bei nafuu ili waweze kufikisha mbolea kwenye maeneo ambayo bado hayajafikiwa.

Fabian alisema kuwa gharama za usafiri wa kufikisha mbolea katika maeneo ya pembezoni mwa nchi imekuwa ni kubwa kwao hivyo wanaiomba selikali kuwasaidia.

Makampuni ya mbolea pia wameiomba serikali kuwasaidia kupata maghala ya kuhifadhia mbolea katika maeneo yaliyo karibu na wakulima.

Akijibu kuhusu maombi ya makampuni hayo Naibu Katibu Mkuu wizara ya Kilimo, Gerad Mweli amesema serikali imechukua hoja hizo na itazifanyia kazi haraka iwezekanavyo ili kuhakikisha kuwa mbolea inawafikia wakulima kwa wakati.

# Mkuu wa Mkoa Kigoma aipongeza TFRA kutatua changamoto uchache wa mawakala mbolea za ruzuku

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Thobias Andengenye ameipongeza Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kwa kuchukua hatua za haraka katika kutatua changamoto ya uchache wa mawakala wa mbolea za ruzuku katika mkoa huo.

Ametoa pongezi hizo leo tarehe 25 Oktoba, 2022 kwa Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dkt. Stephan Ngailo aliyewasili mkoani hapo kwa ziara ya siku 3 ili kujionea mwenendo wa uuzaji wa mbolea kwa wananchi nakutoa taarifa ya kuongezeka kwa mawakala sita huku juhudi za kuendelea kupanua wigo wa uuzaji wa mbolea kwa mawakala waliopo ukiendelea.



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (kushoto) na Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Kati Joshua Ng'ondya (kulia) baada ya mazungumzo mafupi yaliyofanyika katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa tarehe 25 Oktoba, 2022

"Tunashukuru kwa kuona taabu tulizokuwa tunapata kufuatia uchache wa mawakala mategemeo yangu ni kwamba hata hao wachache wataangalia namna watakayofanya ili kupeleka huduma maeneo mengine ya pembezoni" Mkuu wa Mkoa Andengenye aliongeza.

Aidha, Mkuu wa Mkoa Andengenye aliwataka maafisa ugani wa mkoa huo kushiriki katika kutoa taarifa ya maeneo waliyowasajili wakulima na wapo tayari kununua mbolea ili mawakala na kampuni za mbolea ziweze kuwafikishia wananchi mbolea katika maeneo hayo.

Akizungumza katika kikao kifupi na mkuu wa mkoa Andengenye, Dkt. Stephan Ngailo amesema baada ya ofisi yake kupokea changamoto ya kuhusu uchache wa mawakala mkoani humo, ofisi yake imechukua hatua ya



Kikao baina ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dkt. Stephan Ngailo (katikati) na Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Kati, Joshua Ng'ondya ofisini kwa mkuu wa mkoa, tarehe 25 Oktoba, 2022.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo akitoa taarifa ya hatua iliyochukuliwa katika kutatua changamoto ya uchache wa mawakala wa mbolea katika mkoa wa kigoma kwa Mkuu wa Mkoa huo, Thobias Andengenye(hayupo pichani) katika kikao kifupi kilichofanyika ofisini kwa Mkuu wa Mkoa tarehe 25 Oktoba, 2025 .

# Mkuu wa Mkoa Kigoma aipongeza TFRA kutatua changamoto uchache wa mawakala mbolea za ruzuku

kuongeza mawakala pamoja na kuyataka makampuni ya uingizaji wa mbolea kupanua wigo wa usambazaji ili kuondoa kadhia hiyo kwa wananchi.

Ameeleza kuwa, ofisi yake imefanya jitihada ya kuwakutamjisha wafanyabiashara wenye mitaji na kampuni ya OCP na hivyo kuweza kuongeza jumla ya mawakala wapya sita (6) ndani ya wiki moja watakaosaidia kufikisha huduma hiyo karibu na wakulima.

Amebainisha kuwa mawakala hao wapya watauza mbolea katika wilaya za Kasulu TC mawakala wawili, Kibondo DC, Uvinza DC mawakala wawili na Kasulu DC wakala mmoja.

Akizungumzia hali ya upatikanaji wa mbolea katika Mkoa wa Kigoma, Dkt Ngailo amesema,mpaka leo



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Thobias Andengenye akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (hayupo pichani) alipowasili ofisini kwake ili kueleza uwepo wake mkoani humo na kutoa taarifa ya hatua zilizochukuliwa katika kuongeza idadi ya mawakala wa mbolea katika mkoa huo leo tarehe 25 Oktoba, 2025.

maghala yaliyopo mkoani humo yana jumla ya kiasi cha tani 1454.4 za mbolea na kiasi kinachotarajia kufika ndani ya wiki hii ni tani 1492 za mbolea.

Aidha, Dkt. Ngailo amewatoa hofu ya kuwa wakulima kuwa mbolea ya ruzuku itakwisha na kuwataka wanunue mbolea kulingana na mahitaji sawasawa na hatua ya mazao yao huku akikazia kuwa mbolea zitakuwepo msimu wote wa kilimo na wakulima wataendelea kupewa huduma hiyo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (kushoto) akizungumza na wakala wa mbolea za ruzuku wa kampuni ya Yara, Patric Malugu Mirashi ili aweze kupeleka mbolea kwa wakulima wa maeneo ya pembezoni mwa mkoa wa Kigoma jambo alilolipokea na kuahidi kulitekeleza.



Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Stephan Ngailo akioneshwa maeneo yanayotumia mbolea kwa wingi na yale yenye matumizi hafifu kwa mkoa wa kigoma kupitia ramani iliyowekwa katika ukumbi mdogo wa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.

# Ziara ya Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA Ruvuma yazaa matunda

Hivi karibuni Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo amefanya ziara mkoani Ruvuma iliyolenga kujionea mwenendo wa utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku za Mbolea pamoja na kutafuta suluhu ya changamoto wanazokutana nazo wakulima, mawakala wa kusambaz mbolea Pamoja na kampuni za uingizaji mbolea nchini kwa eneo hilo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo akisaini kitabu cha wageni mara baada ya kuwasili ofisi ya Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbinga Mkoani Ruvuma na kupokelewa na Kaimu DAS Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Mwl. Mkuziwa Stewati tarehe 20 Oktoba, 2022.

Katika ziara hiyo iliyoanza Oktoba 5 hadi 7, 2022, Mkurugenzi Dkt. Ngailo alifanikiwa kutembelea halmashauri ya Ruvuma, Madaba, Mbinga na Namtumbo na kuwa na majadiliano na watendaji wa serikali, kampuni za mbolea na mawakala wa mbolea kuona namna watakavyoshiriki katika kuhakikisha mkulima anafikishiwa mbolea karibu na mahala anakofanyia kilimo na hivyo kumpunguzia gharama ya usafiri kufuata mbolea maeneo ya mijini ambako ni mbali na kuongeza gharama za usafiri.

Moja ya matokeo chanya za ziara hiyo ya Dkt. Ngailo ni uwezo wa kumwomba wakala wa kampuni la Mtewele ili aweze kupeleka mbolea wananchi wa Madaba ambao wamekuwa wakifuata bidhaa hiyo Songea mjini na agizo hio kuitikiwa kwa haraka ambapo wananchi hao sasa wanapata huduma hiyo katika wilaya hiyo ya Madaba.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo akizungumza na wakulima waliofulika kununua mbolea katika Ghala la Melt Agro Traactor and Implements LTD Songea mkoani Ruvuma tarehe 20 Oktoba, 2022.

# Ziara ya Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA Ruvuma yazaa matunda


Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo akimweleza jambo mfanyabiashara wa pembejeo za kilimo wa kampuni la Komsango Limited la Mbinga Mkoani Ruvuma alipopita ili kuona namna anavyouza mbolea za ruzuku na kutoa elimu ya namna ya kutumia mfumo wa ruzuku za mbolea kuuza kwa wakulima.

Hayo ni mafanikio makubwa yanatimiza hazma ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kuwasaidia wakulima ili waweze kufanya kilimo chenye tija kitakachoiwezesha nchi kuwa na usalama wa chakula kwani eneo hilo linategemewa zaidi kwa uzalishaji wa chakula nchini.

Aidha, Wilaya ya Namtumbo ilikubwa na changamoto ya kutokuwa na wakala wa anayefikisha mbolea katika wilaya hiyo jambo lililofanyiwa kazi wakati wa ziara hio baada ya Dkt. Ngailo kuzungumza na wakala wa Namtumbo aliyekwama kupeleka mbolea kkwa sababu mbalimbali ikiwemo kutojipanga kwa msimu huu na hivyo jitihada za kupata ghala zilifanyika ili kampuni la YARA na OCP waweze kupata eneo la kutunza mbolea bila gharama na kuwezesha wakulima kupata mbolea kwa wakati.

Ikiwa haitoshi, Dkt. Ngailo alifika katika ofisi za halmashauri ya Mbinga na kujadili changamoto zilizokuwa zikijitokeza hususani za kukosekana kwa stika jambo aliloeleza limepatiwa ufumbuzi kwani imeamriwa gari a mbolea isitoke Dar Es Salaam pasipokuwa na stika kwa ajili ya kuuzia mbolea na hivyo hakutakuwa na haja ya kungojea stika baada ya mzigo kuwasili eneo husika.

Aidha, Dkt Ngailoalitoa elimu ya namna ya kutumia mfumo kuuza mbolea kwa wakala Komsango Limited aliyekuwa tayari kuanza kuuza bidhaa hiyo mara baada ya kukamilisha taratibu zote za uuzaji wa mbolea za ruzuku ikiwa ni Pamoja na kusajiliwa, kuwa na mzigo kwenye mfumo Pamoja na kuwa na stika na hivyo kuanza kutoa huduma kwa wakulima.

Pamoja na kutatua changamoto hizo, Dkt. Ngailo alitoa wito kwa wakulima kununua mbolea kulingana na mahitaji yao na kuueleza umma kuwa mbolea ipo ya kutosha nchini nakuwatoa hofu wakulima kuwa mbolea za ruzuku zina ukomo.

“Mbolea ipo ya kutosha, hata sasa bandarini jijini Dar es Salaam tani elfu 22 za mbolea zinashushwa na zitasambazwa maeneo yote nchini hivyo msiwe na hofu”

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Madaba, Sajidu Idris Mohamed akizungumza mara baada ya kutembelewa na Mkurugenzi Dkt. Ngailo alisema ukanda anaousimamia ni ukanda wa kilimo hivyo mahitaji ya mbolea ni makubwa.

Aidha, alipongeza juhudi za Serikali na Mamlaka kwa ujumla za kuhakikisha maeneo yenye changamoto yanafikishiwa mbolea ikiwa ni pamojana eneo lake ambalo wananchi walikuwa wakifuata mbolea Songea mjini na kuwaongezea gharama ya usafiri.



Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzaniaa (TFRA), Stephan Ngailo, akimsikiliza mfanyabiashara na wakala wa mbolea za ruzuku wa Wilaya ya Namtumbo Said Swamiti walipokutana zilipo ghala za OCP, ETG na Afrisian Ginning LTD walipokutana Mkurugenzi akiwa katika utekelezaji wa majukumu yake hususan yaliyohusu changamoto za kusambaza mbolea za ruzuku kwa wakulima na kumtaka kupeleka mbolea Wilayani Namtumbo.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Stephan Ngailo akimsikiliza msimamizi wa ghala la Melt Agro Tractors and Implements LTD, Arabi Chiwaneke mara baada ya kuwasili na kuona namna anavyowahudumia wateja waliofika ili kununua mbolea ghalani hapo tarehe 20 Oktoba, 2022.



Wakulima wakipakia mbolea kwenye kirikuu baada ya kununua mbolea kwa bei za ruzuku katika ghala la Afrisian Ginning LTD tarehe 20 Oktoba, 2022



Mtumishi wa kampuni ya mbolea ya Melt Agro Tractors and Implements LTD akibandika stika kwenye mbolea aina ya SA tayari kwa ajili ya kuwauzia wakulima waliokuwa wakisubiri kununua mbolea hizo leo tarehe 20 Oktoba, 2022



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) akiwa na watumishi wa OCP katika ghala la kampuni hiyo linalotumika kuhifadhi mbolea tayari kwa ajili ya kuwauzia wakulima na kusambaza maeneo mengine ya mkoa wa Ruvuma alipofanya ziara ya kufuatilia mwenendo wa usambazaji wa mbolea za ruzuku mkoani Ruvuma tarehe 20 Oktoba, 2022.



# Mbolea za ruzuku kuongeza usalama wa chakula nchini - Mkuu wa Mkoa wa Songwe

Mkuu wa mkoa wa Songwe, Waziri Waziri Kindamba amesema mbolea za ruzuku zinazotolewa na Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa msimu wa kilimo 2022/2023 zimelenga kuhakikisha kuna usalama wa chakula nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Waziri Waziri Kindamba akizungumza na hadhara iliyoshiriki kwenye hafla ya ufunguzi wa Maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yanayofanyika kitaifa Mkoani Songwe katika viwanja vya Kimondo wilayani Mbozi

"Usalama wa chakula ni usalama mkubwa kuliko usalama mwingine wowote duniani ili kuwa na amani ni lazima suala la usalama wa chakula lipewe kipaumbele", Kindamba alisisitiza.

Mkuu wa Mkoa Kindamba ametoa kauli hiyo leo tarehe 11 Oktoba, 2022 wakati akifungua maadhimisho ya siku ya mbolea duniani yenye kauli mbiu "Agenda10/30: Matumizi sahihi ya Mbolea ya Ruzuku kwa Kilimo chenye Tija" yanayofanyika kitaifa mkoani Songwe yakiambatana na maonesho kutoka kampuni mbalimbali za mbolea pamoja na taasisi zilizopo kwenye mnyororo wa chakula nchini.




Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo akizungumza wakati wa hafla ya kufungua maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Kimondo vilivyoko wilayani Mbozi Mkoani Songwe tarehe 11 Oktoba, 2022

Amesema, kauli mbiu hiyo imelenga kuonesha dhamira ya Serikali ya Rais Samia katika kuthamini mchango wa Sekta ya Kilimo na kuamua kutenga kiasi cha shilingi bilioni 150 kwa ajili ya kutoa ruzuku za mbolea kwa wakulima ili kuwapunguzia makali ya bei za mbolea na kuwawezesha kulima kilimo biashara.

Akizungumzia kauli mbiu hiyo kwa upande wa wakulima, Kindamba amesema, inawahamasisha wakulima wakubwa kwa wadogo nchini kutumia mbolea katika uzalishaji wa mazao ili kuweza kuzalisha

# Mbolea za ruzuku kuongeza usalama wa chakula nchini - Mkuu wa Mkoa wa Songwe

mazao mengi katika eneo dogo.

Kindamba aliongeza kuwa, ili kuwa na uzalishaji wenye tija ni vyema wakulima wapewe elimu ya matumizi sahihi ya mbolea pamoja na kuelimishwa juu ya afya ya udongo ili wanapotumia mbolea za ruzuku wapate matokea chanya na kuongeza usalama wa chakula nchini.

Akizungumzia juu ya utegemezi wa mbolea kutoka nje ya nchi wa asilimia 90 Kindamba aliitaka Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kuhamasisha uwekezaji wa ndani ili kuwe na uwiano wambolea inayozalishwa nchini kwa asilimia 50 na asilimia 50 kwa zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi ili pesa ya serikali inayotolewa kwa ajili ya ruzuku iwanufaishe wazawa na wawekezaji wa mbolea waliopo ndani ya nchi.

Aidha, Mkuu wa Mkoa Kindamba ameishauri TFRA kupeleka wawekezaji wa viwanda vya mbolea katika mikoa inayojihusisha zaidi na kilimo hususani mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ambako matumizi ya mbolea yapo juu ili bidhaa hiyo iwafikie wakulima kwa wakati na kwa bei himilivu.

Naye, Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Songwe, Eliniko Mkola amesema Ilani ya chama Cha Mapinduzi kipengele cha 3 inaelekeza kuongeza uzalishaji wa mazao na kuongeza usalama wa chakula nchini na ndio maana serikali imeamua kutenga fedha kwa ajili ya ruzuku.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Songwe, Eliniko Mkola akizungumza jambo wakati wa hafla ya kufungua maadhimisho ya Siku ya Mbolea Duniani yaliyofanyika katika viwanja vya Kimondo Mlowo- Mkoani Songwe.

Pia, Mkola ameyataka makampuni yaliyopewa kazi ya kusambaza mbolea za ruzuku nchini kuhakikisha bidhaa hiyo inawafikia wakulima katika maeneo wanakofanyia shughuli za kilimo ili azma ya serikali ya kutenga bajeti kwa ajili ya ruzuku iweze kufikiwa.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TFRA, Dkt. Stephan Ngailo bei elekezi ya mbolea kwa mkulima yeyote nchini si Zaidi ya shilingi elfu 70.

Dkt. Ngailo amefafanua kuwa kwa maeneo ambayo gharama za usafiri ili kufikisha bidhaa hiyo kwa wakulima imekuwa kubwa, kamati za pembejeo za wilaya ziwasilishe maoni ya kiasi kinachozidi ili kuweza kufidiwa kupitia fedha iliyotengwa kwa ajili ya ruzuku.

Mwisho, Dkt. Ngailo ametoa wito kwa wakulima kujisajili kwa wakati ili waweze kunufaika na mbolea za ruzuku pindi msimu unapoanza na si kuanza kujisajili wakati wa msimu kwani hawatapata matokeo wanayotarajia kutokana na kutokufuata kanuni bora za kilimo.

Amesema, kanuni bora za kilimo zinamtaka mkulima kuandaa shamba kwa wakati, kupanda na kukuzia kwa kutumia mbolea bora huku akizingatia matumizi sahihi ya mbolea, na kupalilia kwa wakati.

# Matukio mbalimbali wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mbolea









# Wakala wa mbolea watakiwa kuongeza vituo vya mauzo kuwafikia wakulima vijijini

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo amewataka mawakala wa mbolea za ruzuku kuongeza watendaji ili kuweza kuhudumia wakulima wengi zaidi wanaofika kununua mbolea hizo.



Mkuu wa Wilaya ya Kasulu Kanali Isaac Anthony Mwakisu (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (kushoto) na Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Kati Joshua Ng'ondya walipofika ofisini kwake kueleza uwepo wake wilayani hapo kufuatilia mwenendo na upatikanaji wa mbolea za ruzuku wilayani humo

Amesema, kufuatia kuwa mfumo unaotumika kuuza mbolea ni mpya wafanyabiashara wanakwenda taratibu hivyo kuongeza watumishi kutasaidia kupunguza foleni ya wakulima kwenye maghala na maduka ya mbolea huku tukiamini msimu ujao changamoto hii itakuwa imepunguzwa kwa kiwango kikubwa.

Dkt. Ngailo ametoa kauli hiyo hivi karibuni kwa nyakati tofauti alipokuwa akizungukia maghala na maduka ya pembejeo za mbolea katika Halmashauri za Wilaya ya Kasulu, Buhigwe, Kibondo na Kakonko mkoani Kigoma na kukuta wananchi wengi wakiwa kwenye foleni ili kupata mbolea huku kukiwa na wahudumu wachache.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha na Wakala wa Mbolea wa kampuni la OCP Yotham Mbwila Tanditse Afisa Mauzo wa OCP Benezeth katonkola (kushoto kwake) na Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Kati Joshua Ng'ondya (wa kwanza kulia) wakati wa ziara yake ya kukagua mwenendo na upatikanaji wa mbolea za ruzuku katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Mkoani Kigoma tarehe 26 Oktoba, 2022

Akizungumza na wakurugenzi wa halmashauri husika pamoja na maafisa kilimo, Dkt. Ngailo alishauri kuwa, kwa wakulima walio kwenye vyama vya ushirika (Amcos) wanaweza kununua mbolea kupitia viongozi wao kwa kuzingatia taarifa walizowasilisha wakati wa usajili na hivyo kusaidia kupunguza msururu wa wakulima kwenye maduka na maghala ya pembejeo.

Ili kutatua changamoto ya wakulima kusafiri mwendo mrefu kufuata mbolea, Dkt. Ngailo alifanya juhudi ya ziada kuhakikisha anawashirikisha viongozi katika ngazi za halmashauri ili kuwezesha upatikanaji wa maghala kwa ajili ya kuwapunguzia

# Wakala wa mbolea watakiwa kuongeza vituo vya mauzo kuwafikia wakulima vijijini

wafanyabiashara gharama za uendeshaji.

Pamoja na hayo, Dkt. Ngailo amewataka mawakala wa mbolea kusogeza huduma kwenye maeneo ya pembezoni ili kuwapunguzia wakulima adha ya kufuata huduma hiyo maeneo ya mjini jambo linalosababisha kuwa na msururu mrefu wa wananchi wanaosubiri kupata huduma hiyo.

Akieleza maeneo yaliyoongezewa mawakala katika Wilaya ya Kasulu na Buhigwe, Dkt. Ngailo alisema ni pamoja na Nyarubaza, Kajana, Mbanga na manyovu kwa Wilaya ya Buhigwe ambapo wakala Sebastian Mganya na Yotham Mbwila watafikisha huduma katika maeneo hayo.

Aidha, kwa halmashauri ya Kibondo, huduma zitasogezwa katika tarafa za Busunzu, mabamba na Nyaruyoba na wakala Plan General Supply na Boniface Munya na hivyo kupunguza kadhia kwa wakulima.



Mkuu wa Wilaya ya Kibondo A. J. Magwaza (katikati) akizungumza jambo na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (kushoto) na wataalama walioongozana na mkurugenzi alipofika ofisini kwa mkuu wa Wilaya kueleza hatua zilizochukuliwa katika kutatua changamoto ya mbolea katika wilaya hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza mawakala wa mbolea wilayani humo.

Kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko kulikuwa na wakala mmoja ambye ni _Plan general supply_ ambapo wataongezeka mawakala wawili ambao ni Sebastian Mganya wa kampuni la YARA na Boniphace Munya wa kampuni la OCP hivyo kupunguza changamoto kwa eneo hilo.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Kanali Isaac Anthony Mwakisu aliishukuru Mamlaka kwa mwitikio wa kuongeza mawakala na kuona umuhimu wa kufika ili kutatua changamoto za mbolea katika maeneo yao na kuiomba mamlaka kuendelea kutatua changamoto za mfumo ili zoezi liende vizuri.

“Tunashukuru tumeona mwitikio wa kuongeza mawakala lakini tunaomba mfumo ufanye kazi, mkiboresha mfumo itarahisisha na kupunguza foleni” Kanali Mwakisu alisisitiza.



Mkuu wa Sehemu ya Kilimo Wilayani Kibondo, Yahya Mtongori akieleza jambo wakati wa kikao baina ya Mkuu wa Wilaya Kanali A. J Magwaza (hayupo pichani) na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Dkt. Stephan Ngailo tarehe 27 Oktoba, 2022. Kulia ni Kaimu Meneja wa TFRA Kanda ya Kati Joshua Ng’ondya.





Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dkt. Stephan Ngailo (mwenye kofia) akizungumza na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Buhigwe Essau Hosea Ngoloka Dkt. Ngailo alipofika na kuzungumza naye juu ya upatikanaji wa ghala kwa ajili ya kuhifadhia mbolea na kuuza kwa wakulima ili kuwapunguzia wakulima hadha yakufuata mbolea maeneo ya mbali.













# Mfanyabiashara aliyehujumu juhudi za serikali mbolea za ruzuku atiwa hatiani Moshi

Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Said Mtanda ameamuru kutiwa nguvuni kwa mfanyabiashara na wakala wa mbolea za ruzuku la Red Star Service ajulikanaye kwa jina la Musa Idowa baada ya kubainika kuuza mbolea iliyodaiwa kuwa feki na isiyolingana na vifungashio vilivyotumika kuweka mbolea hiyo.


Aidha, mfanyabiashara huyo, alibainika kuweka mbolea ya aina moja katika vifungashio vilivyowekwa lebo ya SA, DAP, NPK, UREA huku akidai yote ni Urea.

Mkuu wa Wilaya Mtanda, alitoa maelekezo hayo tarehe 23 Oktoba, 2022 mara baada ya kujiridhisha kuwa mfanyabiashara huyo anauza mbolea isiyo halisi (feki) jambo linalorudisha nyuma juhudi za serikali za kumwezesha mkulima kuzalisha kwa tija.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania ( TFRA) Kanda ya Kati, Gothard Liampawe akieleza kwa njia ya simu na kutoa taarifa ya kupatikana kwa wakala anayejishughulisha na biashara hiyo kwa udanganyifu wilayani Moshi.

Aidha, mfanyabiashara huyo alibainika akikusanya namba za wakulima na kuuza mbolea badala ya kutumia mfumo unaowaelekeza wauzaji wote wa mbolea nchini kuutumia kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2022/2023.

Kwa upande wake, Meneja wa Kampuni ya YARA kanda ya Kaskazini, Novatus Joseph Salala alieleza kuwa kifungashio kilichotumika



# Mfanyabiashara aliyehujumu juhudi za serikali mbolea za ruzuku atiwa hatiani Moshi

kuweka kilichosemekana ni mbolea ni cha YARA EAST AFRICA kwa upande wa Kenya lakini kilichokutwa ndani hakikuwa mbolea ya UREA inayouzwa na kusambazwa na kampuni hiyo.

Katika wakati mwingine, wakaguzi kutoka TFRA wakiendelea na ukaguzi katika duka la Chanya Agro Success lililopo Mbuyuni wakaguzi wa TFRA walibaini mfanyabiashara huyo akiuza mbolea kwa bei ya shilingi 80,000 kwa mbolea ya SA, shilingi 90,000/= kwa mbolea ya CAN na shilingi 130,000/= kwa mbolea ya YARA WINNER ambayo ni kinyume cha sheria na maelekezo ya serikali yanayowataka wafanyabiashara kuuza mbolea kwa bei ya chini ya shilingi 70,000 kulingana na aina ya mbolea.

Lengo la Serikali kuja na mpango wa ruzuku za mbolea ni kuhakikisha kuwa mkulima anapata mbolea bora ili kuweza kuzalisha kwa tija na kuuza kwa kutumia mfumo stahiki ulioandaliwa na serikali hivyo makosa yaliyofanywa na mfanyabiashara Musa Idowa yanakwamisha juhudi za serikali ktika kutekeleza kauli mbiu ya 10/30 kutokana na kuathiri uzalishaji.




Akihitimisha maelezo yake, Kaimu Meneja Liampawe amewahakikishia wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuwa ofisi yake itaendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara na wafanyabiashara wasio waaminifu watabainika na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa kanuni, taratibu na sheria.

Habari katika picha wakati wa ziara ya Mkurugenzi mtendaji kuzungumza na viongozi wa halmashauri za Misenyi, Ngara, Bukoba, Biharamulo na Muleba ili kupata maghala yasiyo na gharama kwa ajili ya kuwasogezea mbolea wakulima wa maeneo hayo na kupinguza umbali wa kwenda kuifuata bidhaa hiyo.








Habari katika picha wakati wa ziara ya Mkurugenzi mtendaji kuzungumza na viongozi wa halmashauri za Misenyi, Ngara, Bukoba, Biharamulo na Muleba ili kupata maghala yasiyo na gharama kwa ajili ya kuwasogezea mbolea wakulima wa maeneo hayo na kupinguza umbali wa kwenda kuifuata bidhaa hiyo.











